BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 28 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2024/2025.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

177. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa ambazo bado hatujafikia kiwango cha mafanikio ya kuridhisha, suala la kupanda na kutunza bustani za barabarani, limeendelea kuwa na mapungufu mengi, na kimsingi bado hatujafanikiwa ipasavyo.

Je, Wizara yako imefanya tathmini zipi za kujua kuna tatizo gani mpaka tukawa tunashindwa kuzipanda, kuzihudumia na kuzitunza bustani zetu za barabarani.

178. Mheshimiwa Haji Shaaban Waziri (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, ni lini Wizara yako imefikiria na kuamua kupanda bustani ya asili katika barabara zetu, ikiwa ni pamoja michaichai, milangi langi, miasumini, miwardi na bustani nyengine za asili.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

23. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, ni lini Wahasibu wa Serikali kwa upande wa Pemba watawezeshwa kwa lengo la kufunga hesabu zinazojitegemea (segment financing).

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

89. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda mrefu sasa, nchi yetu inaendelea kukumbwa na tatizo la utoro mashuleni mwetu.

Je, takwimu ziko vipi juu ya wanafunzi wanaotoroka shuleni.

90. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa kuongeza juhudi ya kuwainua wananchi wetu kielimu. Hata hivyo, suala la kuzingatia umahiri wao katika masomo ni jambo lenye umuhimu mkubwa.

Je, Wizara yako inatumia utaratibu upi utakaosaidia kupima umahiri wa wanafunzi wetu.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

43. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na mwitikio mdogo wa agizo la Serikali la kuzitaka taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zao na kufanyiwa kazi na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (The Zanzibar Government Printing Press (ZGP)), kiasi kwamba ZGP hukosa kazi za kuiwezesha kusimama na kutimiza malengo ya kuasisiwa kwake.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha taasisi nyingi za Serikali kutotii agizo hili la kupeleka kazi zao ZGP.

(b) Je, ni ipi mikakati mipya ya kuhakikisha kwa asilimia 100 taasisi za Serikali zinatii agizo hili.

(c) Je, kwa miaka mitano iliyopita (2018/2019 - 2022/23), ni kazi ngapi kwa wastani zilitarajiwa kupelekwa ZGP kutoka katika taasisi za Serikali na ngapi hasa zilipelekwa.

128. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Licha ya kukuwa na kuimarika kwa lugha adhimu ya kiswahili duniani Zanzibar tumekuwa na uhaba wa wataalamu katika taaluma ya tafsiri na ukalimani.

Je, ni jitihada gani ambazo Wizara yako inazichukuwa ili kuona kwamba tunazalisha wakalimani na watafsiri wa kutosha.

Wizara ya Afya:

19. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Serikali imejenga hospitali za daraja mbali mbali hapa nchini, na kwa kuwa mikataba ya kimataifa imeweka kiwango maalum cha wagonjwa ambacho kila daktari anapaswa kutibu kwa siku.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini juu ya idadi ya madaktari hususan madaktari bingwa waliopo nchini.

(b) Kama tayari imefanya, je hakuna uhaba wa watumishi hao.

107. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini iko vipi juu ya idadi ya vifo vya kinamama vinavyotokana na maradhi yasiyoambukiza.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

126. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Asilimia 90 ya wanaojishughulisha na kilimo cha mwani ni kina mama. Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwaondolea wakulima hawa changamoto ya muda mrefu ya bei ndogo katika soko la mwani.

133. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hivi sasa dhana ya falsafa ya uchumi wa buluu imekuwa, imezoeleka na imeeleweka vizuri kwa wananchi.

Je, ni lini Wizara itakamilisha mswaada wa kamusi la viumbe vya baharini ili kuendana na wakati huu wa uchumi wa buluu.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

39. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ilielezwa kwamba barabara ya Kiungoni – Tovuni ilikuwa ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa tuta lenye urefu wa mita takriban 400 la kuzuia maji ya bahari kuingia kwenye maeneo ya kilimo katika eneo la Tovuni, shehia za Kiungoni na Mjananza (Pandani) kupitia Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani ya Zanzibar. Hata hivyo, hadi sasa barabara hiyo haijajengwa.

(a) Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa na lini itakamilika.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kutoka kwenye fedha ya mradi uliofadhiliwa

na Benki ya Dunia (WB) kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

(c) Je, ni lini barabara nyengine iliyoanza kusafishwa ya Kiungoni –Tovuni itaanza kujengwa na lini itakamilika.

141. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ujenzi wa barabara ya Chake - Wete yenye urefu wa kilomita 22.1 unaendelea, ingawa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusu kutolipwa fidia zao hadi sasa.

(a) Je, ni wananchi wangapi ambao tayari wameshapokea fidia zao tangu kuanza kwa zoezi la kupisha ujenzi wa barabara hii.

(b) Ni idadi gani ya wananchi ambao bado hawajapokea fidia zao hadi sasa na Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata fidia zao stahiki kwa kupisha ujenzi wa barabara hii.

(c) Serikali inatumia njia gani za tathmini ya mali (majengo) ili kuhakikisha malipo ya fidia yanafanyika kwa haki na kwa usahihi kwa wananchi wanaopisha miradi ya ujenzi wa barabara kama hii ya Chake – Wete.

174. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali kujenga barabara mbali mbali mijini na vijijini, kumejitokeza tabia iliyozoeleka ya barabara za mjini pekee,kwa maana ya Mkoa wa Mjini Magharibi kufagiwa na kutunzwa kwa bustani na taa za pembeni, lakini jambo hili halifanyiki kwa barabara za vijijini, ikiwa ni pamoja na jimbo la Uzini.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopekea barabara kuu za jimbo la Uzini kutofagiliwa na kuwekwa taa za pembeni.

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuzifagia na kuziwekea taa za pembeni barabara hizo.

(c) Serikali inazitunza vipi barabara hizo, ukiachia mbali kukatwa majani pembeni, tena kwa kusuasua.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

Zanzibar,
28 Februari, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.